JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

S. L.P. 38
GEITA
Simu: 028-2520004
Nukushi: (028) 2520040
Baruapepe: rbcgeita@pccb.go.tz
Website: www.pccb.go.tz

GEITA – APRILI 15, 2020.

TAARIFA KWA UMMA

KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

TAKUKURU MKOA WA GEITA YAFANYA OPERESHENI ZA SHILINGI 2,017,374,792.95/= KUOKOA SHILINGI 219,581,500/=.

NDUGU WANAHABARI.
Ninapenda kuchukua fursa hii kuwashukuru sana kwa kuitikia wito wetu na kuja kushiriki kwenye mkutano huu ulioandaliwa kwa ajili ya kuuhabarisha umma juu ya kazi ambazo zimetekelezwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Geita katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Machi, 2020. Karibuni sana ofisi ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Geita.

NDUGU WANAHABARI.
Katika kipindi cha Januari hadi Machi, 2020 Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Geita, imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya mwaka 2007 kwa kushirikiana na ofisi zake zote za wilaya na wananchi kwa pamoja.

Katika kipindi hicho TAKUKURU Mkoani Geita imefanya na inaendelea na Operesheni mbalimbali za kufuatilia tuhuma za ubadhilifu wa fedha kiasi cha S**hilingi 2,017,374,792.95/=** za Vyama vya Ushirika wa wachimbaji wadogo wadogo vya NYAMATAGATA; kiasi cha **Shilingi 1,832,241,151.76/=,** IKUZI Shilingi **63,180,102.24/=** pamoja na chama cha kuweka na kukopa (GEITA SACCOS) **Shilingi 121,953,538.95/=**.

Aidha jumla ya fedha kiasi cha **Shilingi 52,581,500/=** zimeokolewa kupitia chunguzi mbalimbali kwa mchanganuo ufuatao kisekta; **Fedha taslimu** Tamisemi **(Shilingi 7,030,000/=),** Afya **(Shilingi 10,107,000/=)**, Elimu **(Shilingi 500,000/=)**, Uchaguzi **(Shilingi 11,395,000/=)**, Misitu **(Shilingi 1,750,000/=)**, AMCOS (**Shilingi** 6,000,000/=), Mawasiliano **(Shilingi. 80,000/=)**, Sekta binafsi/Mikopo vikundi **(Tsh. 682,000/=),** CSR **(Tsh. Tsh 14,327,500/=)** na Maji **(Shilingi. 75,000,000/=)**. Pia Taasisi imeokoa fedha kwa njia ya **udhibiti (Non Cash**) jumla ya shilingi **92,170,000/=** ambazo ni kutoka sekta ya misitu **(Shilingi 100,000/=), Ardhi (Shilingi. 92,000,000/=) na** Mahakama **(Shilingi 75,000/=)**.

NDUGU WANAHABARI
Katika kipindi husika tumetekeleza majukumu mengine kama ifuatavyo;

1.0. UCHUNGUZI NA MASHTAKA

Katika kipindi husika zimepokelewa jumla ya Taarifa 81 za malalamiko dhidi ya rushwa na makosa mengine. Taarifa zilizopokelewa zinahusisha, Serikali za mitaa –16, Mahakama – 09, Afya –08 Utawala –08, Elimu –07, Ushirika/kilimo–06, Taasisi za kifedha– 06, Ardhi-05, Ujenzi – 04, Madini –02, Polisi – 02, Misitu/Maliasili –02, Sekta binafsi –02, Nishati/umeme –01 na Mawasiliano-01.

Baada ya taarifa hizo kufanyiwa uchunguzi wa awali, ofisi imefungua jumla ya majalada ya uchunguzi 09, taarifa 05 zimehamishiwa idara nyingine, taarifa 23 zilitolewa ushauri na hatua za kiutawala na taarifa 41 zinaendelea kufanyiwa kazi. Katika kipindi hicho jumla ya majalada 04 uchunguzi wake umekamilika na majalada 02 yalipata kibali cha mashtaka ambapo tayari watuhumiwa wamefikishwa mahakamani.

Katika kipindi cha Januari hadi Machi, 2020 Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Geita ilifungua kesi mpya 06 mahakamani ambapo watuhumiwa 07 wamesomewa mashtaka.

Aidha kwa kipindi hicho ofisi imeendesha kesi 35 mahakamani, ambapo kati ya kesi hizo, zilizotolewa maamuzi ni 08 ambapo kesi 06 tulishinda na kesi 02 tulishindwa. Taratibu za kukata rufaa zinaendelea kwa kesi zilizoshindwa.

2.0. UELIMISHAJI UMMA.

Wananchi wameendelea kuelimishwa kuhusu madhara ya rushwa na nafasi yao katika mapambano dhidi ya rushwa ambapo:

- Semina 51 zimetolewa.
- Mikutano ya hadhara 28 imefanyika katika vijiji na kata za mkoa wa Geita ikiwa ni sehemu ya kuelimisha wananchi kuchagua viongozi bora na sheria ya uchaguzi katika kipindi cha kampeni za uchaguzi mkuu 2020 pamoja na elimu ya kampeni ya UTATU, VUNJA UKIMYA KATAA RUSHWA YA NGONO na matumizi ya TAKUKURU APP.
- Klabu 117 zimeimarishwa.
- Klabu 175 zimefunguliwa.
- Taarifa kwa vyombo vya habari 07 zimetolewa.
- Maonesho 05 yamefanyika
- Jumla ya makala 04 zimeandaliwa ikiwa ni pamoja na mkutano 01 na waandishi wa habari umefanyika.
- Aidha jamii imeelimishwa kupitia machapisho **2,575** yenye ujumbe wa kukemea vitendo vya rushwa ambayo yamegawiwa kwa wananchi vijijini/mjini na watumishi wa sekta za Umma na binafsi ikiwa ni pamoja na kuelimisha umma kwa kuendesha kipindi cha redio **01** kuhusu makosa ya rushwa katika uchaguzi.

3.0. UZUIAJI RUSHWA.

Katika kipindi cha Januari – Machi, 2020 TAKUKURU mkoa wa Geita imetekeleza jukumu la uzuiaji rushwa kwa kufanya uchambuzi wa mifumo mitano (05) katika sekta tatu (03) ambazo ni vyama vya ushirika (AMCOS), nishati (REA) na wanyamapori.

Pia warsha mbili (02) zilifanyika kwa lengo la kuweka maazimio ya namna ya kuziba mianya ya rushwa iliyobainika katika uchambuzi wa mifumo sambamba na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio sita (06) yaliyofikiwa.

Aidha miradi ya maendeleo yenye thamani ya **Shilingi 7,866,100,000/=** imefuatiliwa katika sekta za Afya, Elimu na Ujenzi. Kati ya fedha hizo Shilingi **4,500,000,000/= bilioni** zinatokana na miradi ya Corporate Social Responsibility (CSR) kutoka sekta ya madini.

KUELEKEA UCHAGUZI MKUU 2020.

NDUGU WANAHABARI:

Sote tunafahamu kuwa mwaka huu mwezi Oktoba, 2020 tutakuwa na Uchaguzi Mkuu. Uchaguzi huu unapaswa kuendeshwa na kusimamiwa kwa uadilifu na umakini mkubwa kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu ili haki, usawa, uhuru na demokrasia viweze kustawi, kuendelezwa na kudumishwa.

Rushwa katika Uchaguzi ni hatari na inaweza kuleta madhara kwa Taifa kwani viongozi wala rushwa au watoa rushwa hawataweza kuisimamia nchi katika misingi ya haki, usawa, uwazi, uwajibikaji na uzalendo. Vilevile wananchi wapokea au watoa rushwa hawawezi kuhoji masuala mbalimbali ya maendeleo kwa viongozi wao. Kwa kuzingatia umuhimu wa uchaguzi TAKUKURU tumejizatiti kufuatilia kwa umakini hatua kwa hatua uchaguzi huu, watakaojihusisha na vitendo vya rushwa hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Tunaomba vyombo vya habari visaidie pia kuwafichua wagombea watoa rushwa kwa kutoa taarifa TAKUKURU kwani mapambano dhidi ya rushwa ni jukumu letu sote. Vyombo vya habari ninaomba mtumie fursa mliyo nayo ya kuifikia jamii kwa kuwaelimisha kupitia vyombo vyenu ili wananchi waweze kutambua thamani na umuhimu wa kura zao katika kupata viongozi walio bora.

4.0. MWISHO

Mikakati ya TAKUKURU Mkoa wa Geita kwa kipindi cha Aprili – Juni, 2020 ni kuendelea kutatua kero za wananchi zinazohusiana na vitendo vya Rushwa, kutoa elimu ya rushwa kwa wananchi ili waelewe haki na wajibu wao katika kupata huduma, kuendelea kuwaelimisha watumishi wa sekta za Umma na binafsi kuwa waadilifu katika utekelezaji wa majukumu yao.

Pia napenda kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa kukubali kuja kunisikiliza na hasa tukizingatia umuhimu wa shughuli yenu ya habari, napenda kutoa wito kwenu kuendelea kutoa elimu juu ya adui rushwa kwa jamii, TAKUKURU inawaomba mkaendelee kuwa mabalozi madhubuti wa mapambano dhidi ya rushwa.

Wito wetu kwa wananchi waendelee kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa, kuwa waadilifu kwa kutojihusisha na vitendo vya kuomba na kupokea rushwa, washiriki pia kutoa taarifa za vitendo vya rushwa TAKUKURU kwa kupiga simu ya bure 113 au kutuma sms 113 au kupiga *113# au kupitia TAKUKURU APP.

"Kwa pamoja tukishirikiana Tanzania bila Rushwa Inawezekana"

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA

imetolewa na:

Leonidas R. Felix
MKUU WA TAKUKURU (M) GEITA